

Dickson John ni mwandishi wa vitabu mbalimbali vya ujasiriamali na mwalimu elimu binafsi za maisha. Uandishi ni ndoto ambayo amekuwa nayo tangu zamani na hivi sasa ameamua kuiweka katika vitendo. Miongoni mwa vitabu alivyoandika ni pamoja na:-

- ❖ Kiwanda Mkononi.
- ❖ Fanikisha Ndoto Yako.
- ❖ Una nini Mkononi?

## **SHUKRANI**

Napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema ambaye amenijalia heri hadi kufika hatua ya kuandika kitabu hiki, ingawaje haikuwa kazi rahisi lakini yeye kanisimamia hadi kuandika utimilifu wote wa kitabu hiki.

Namshukuru mama yangu mpenzi ambaye kwa dua na sala zake nimeweza kukamilisha uandishi wa kitabu changu cha tatu baada ya kiwanda mkononi na Fanikisha ndoto yako. Ndugu zangu wote katika mwili na katika kristo.

Nawashukuru watu kutoka Peace Stationery, wachapaji wa kitabu hiki ambao wamenipa ruksa kutumia vifaa vyao hadi kumaliza uandishi wa kitabu hiki. Mwenyezi Mungu mwingi wa heri awajalie Baraka na kuzidi kusonga mbele.

Namshukuru pia rafiki yangu Mwl. Darius Joseph ambaye amekuwa mchango mkubwa katika kuhariri maneno ya kitabu hiki, Mungu amjalie heri na fanaka katika maisha yake

Mwisho nawashukuru wale wote ambao wamekuwa na msaada mkubwa kwangu, aidha kwa maoni na ushauri wao au kununua vitabu vyangu. Mungu awabariki sana na kuzidi.

*Ikiwa haujasoma kitabu changu kitiwacho **Fanikisha ndoto yako**, basi nikusihii ukitafute kwa kutumia mawasiliano yaliyo nyuma ya kitabu hiki. Kwa kufanya hivyo utakuwa umechangia kufikisha elimu kwa wale wasiofikiwa. Mungu akubariki sana.*

Yaliyomo

WAKFU ..... **Error! Bookmark not defined.**

SHUKRANI..... - 1 -

MANENO YA UTANGULIZI..... - 3 -

SURA YA KWANZA

MAISHA NA CHANGAMOTO ..... **Error! Bookmark not defined.**

WEWE NI WA THAMANI-.....

KIMFAACHO MTU CHAKE- ..... **Error! Bookmark not defined.**

SABABU NI WEWE-..... **Error! Bookmark not defined.**

SHUKURU ULICHONACHO HUKU UKIPIGANIA UNACHOKITAKA- ... **Error! Bookmark not defined.**

SURA YA PILI

ELIMU-..... **Error! Bookmark not defined.**

MIFUMO YA ELIMU RASMI-..... **Error! Bookmark not defined.**

MATUNDA MAKUU YA ELIMU- ..... **Error! Bookmark not defined.**

ELIMU YENYE MANUFAA-..... **Error! Bookmark not defined.**

ONGEZA THAMANI KATIKA ELIMU YAKO-.....

SURA YA TATU.

-KIPAJI NA UBUNIFU-.....

-NAMNA YA KUTAMBUA KIPAJI CHAKO-.....

-ONGEZA THAMANI KATIKA KIPAJI CHAKO- ..... **Error! Bookmark not defined.**

SURA YA NNE**Error! Bookmark not defined.**

MAZINGIRA-..... **Error! Bookmark not defined.**

FURSA KATIKA MAZINGIRA- ..... **Error! Bookmark not defined.**

ONGEZA THAMANI KATIKA MAZINGIRA YAKO-..... **Error! Bookmark not defined.**

SURA YA TANO

AJIRA- .....  
-ONGEZA THAMANI KATIKA AJIRA- .....

SURA YA SITA.....

-UJASRIAMALI NA KUJIAJIRI-..... **Error! Bookmark not defined.**

SURA YA SABA

BIASHARA NA UWEKEZAJI.....-

REJEA.....

## MANENO YA UTANGULIZI

Na: Dickson John

*“Usilie juu ya kile ambacho huna; tumia vizuri kile ulichonacho” - R. Mengi*

**W**ingi wa rasimali za Tanzania haimanishi ndio mafanikio ya wakazi wake. Katika nchi yetu pendwa ya Tanzania ina rasimali za kutosha kuweza kutufanya kuishi kwa raha kama ilivyokuwa Libya enzi za Rais Gaddafi. Hebu fikiri idadi ya mbuga za wanyama, mito, bahari na vivutio mbalimbali ambavyo ni rasilimali, inatajwa kuwa Tanzania ni nchi ya pili duniani kwa kuwa na vivutio vingi vya utalii, ikitanguliwa na nchi ya Brazil. Katika mtazamo huo huo, watu hususani vijana wana vitu ambavyo haviwasaidii katika maisha yao. Tunao uwezo ndani yetu ambao tunaweza kuutumia tukafika mbali. Cha ajabu hautusaidii kufkia mahali tunapotaka.

Kutokana na hilo ndipo ikanisukuma kuwaandikia vijana wenzangu namna ambavyo wanaweza kutumia kile walichonacho na kujifanikisha katika maisha. Vijana wengi hubaki na lawama, wakilaumu wazazi na wengine serikali – kwa kukosa ajira, au kutojengewa misingi mizuri toka utotoni. Lakini mimi nadhani sio sababu ya kutufanya kulaumu, tunachotakiwa ni kujigundua sisi mapema, tuna nini ambacho kinaweza kuwa na manufaa kwetu. Nini hicho ndipo tujifunze namna ya kutumia kile tulichonacho. Hatua moja huanzisha nyingine, safari ya maili mia huanza na hatua moja. Hata wewe unaweza kutumia kile ulichonacho nacho kikakusaidia.

Una nini Mkononi – Nguvu ya ulicho nacho, ni kitabu kinachojaribu kuelezea kwa sehemu kuhusu mambo mbalimbali yamahusuyo binadamu, husasani katika nyanja za mafanikio na namna ambavyo anaweza kutumia kile alichonacho kutatua changamoto zake. Jina la kitabu UNA NINI MKONONI limetokana na kitabu kimoja kutoka katika biblia, kiitwacho KUTOKA 4;1-8, kitabu cha pili katika mpangilio wa vitabu katika Biblia, - (nadhani pia kinapatikana katika Quran- kwa waislamu) imeandikwa hivi *‘Musa akajibu akisema, lakini, tazama, hawataniamini, wala hawatasikia sauti yangu, maana watasema, Bwana hakututokea. Bwana akamwambia, ni nini hiyo uliyo nayo mkononi mwako? (Tafsiri rahisi- una nini mkononi) Akasema, Ni fimbo. Akamwambia itupe chini; akitupa chini, nayo ikawa nyoka; Musa akakimbia mbele yake. Bwana akamwambia Musa, nyosha mkono wako kamshike mkia, (akaunyosha mkono wake akamshika, naye akageuka kuwa fimbo mkononi mwake;) ili kwamba waweze kusadiki ya kwamba Bwana , Mungu wa Ibrahimu, Mungu wa Isaka, Mungu wa Yakobo, amekutokea.....’* – **KUTOKA 4;1-5.**

Katika Nukuu hiyo tunaweza kuitafsiri kwa namna tofauti kulingana na uelewa na mazingira unayotafsiri. Katika kuhusianisha na jina la kitabu, ninaweza kusema kwamba Mungu alitaka kumuonyesha Musa namna ya kutumia kile kitu alichonacho, namna ya kutumia fursa aliyonayo. Musa aliulizwa una nini mkononi mwako, na mkononi mwake alikuwa na fimbo pekee. Na hicho ndicho

Piga hatua moja yenye thamani

alichoulizwa ili atoe jibu, Mungu akamwambia kupitia fimbo hiyo unaweza kufanya maajabu mpaka watu wakaamini kuwa amemtokea, maana Musa alikuwa na mashaka sana kuhusu kukubaliwa na wale watu anaowaendea, lakini Mungu akamfungulia njia kupitia kile alichokuwanacho. Mbali na nguvu ya maombi aliyokuwa nayo Musa, miujiza mingi inaonekana kutendeka kwa fimbo aliyokuwa nayo mkononi mwake. Alipiga maji yakawa damu, mavumbi yakawa chawa, bahari ya shamu ikagawanyika, yote ni kutokana na kutambua uwezo aliokuwa nao kwa wakati ule kupitia fimbo.

Kile ulichonacho mkononi haina maana kwamba ni kile ulichokishikiria hapana isipokuwa ni kile ulichonacho katika maisha yako. Waswahili waliwahi kusema *‘heri moja mkononi kuliko kenda (9) nenda uje’* walitambua nguvu ya kitu unachomiliki kuliko usichomiliki. Cha kwako kina thamani kuliko kisicho cha kwako. Ulichonacho sasa ni bora zaidi kuliko kile unachokitarajia. Na hii ndio maana ya jina la kitabu **una nini Mkononi**. Tutajadili mambo mbalimbali ambayo tunayo mikononi mwetu, nikusihi tu twende pamoja nawe utagundua na kufunguka kama Musa alivyofunguka. Kufanikiwa kwa mwanadamu kunategemeana na kile kitu alichonacho, na namna anavyokitumia katika maisha yake ili kufikia mafaniko.

Moja ya jambo ambalo kila mtu analo ni “kipaji”, katika kitabu hiki tutaangalia kwa kina namna ya kugundua kipaji chako, namna ya kukitumia kipaji chako lakini pia mazingira ya kukitumia kipaji chako.

Jambo lingine ambalo mtu anaweza kuwa nalo ni Elimu, ndani ya elimu kuna vitu viwili vikuu ambavyo mimi naviona vinapaswa kupatikana katika elimu, moja ni Taaluma, Taaluma ni ujuzi tunaoupata kutokana na kufundishwa yamkini darasani au mahali pengine. Pili ni Maarifa, Maarifa ni uwezo ambao unaoupata kutoka katika kujifunza. Hebu zingatia kitu fulani hapa, kuna tofauti kati ya kufundishwa na kujifunza, unaweza ukafundishwa lakini usijifunze, sasa kama utafundishwa nawe ukajifunza matokeo yake ni kwamba utatoka na taaluma pamoja na maarifa katika elimu yako.

Jambo lingine ni fursa kulingana na mazingira, karibia matajiri wote duniani wanapendekeza kutafuta fursa ndani ya changamoto. Kwamba ili ufanikiwe zaidi lazima uwe umetatua changamoto fulani katika jamii. Wape watu kitu wanachohitaji au huduma wanayoihitaji – hapo ndipo ilipo siri ya pesa yako, au mafanikio yako. Katika kitabu hiki tutajadili namna ya kutumia fursa inayopatikana katika mazingira yako. Katika mazingira yetu zipo fursa ambazo bado hakuna mtu amezifikiria, zinakusubiri wewe ili uweze kuzitatua, *“Anzia ulipo. Tumia ulichonacho. Fanya unachoweza”* – Arthur Ashe

